Jina: …….. Nambari yako: ……...

Sahihi ya mtahiniwa……...

Tarehe: ……..

102/2
KISWAHILI
Karatasi ya 2
LUGHA
Machi/Aprili 2011
Muda : Saa 2 ½

MTIHANI WA MWIGO WA PAMOJA WA MOKASA

Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari – Kenya
102/2
KISWAHILI
Karatasi ya 2
LUGHA
Machi/Aprili 2011
Muda : Saa 2 ½

Maagizo :

(a) *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
(b) *Tia sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
(c) *Jibu maswali yote. Andika majibu yako katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
(d) ***Karatasi hii ina kurasa 11 zilizopigwa chapa.***
(e) ***Watahiniwa lazima waangalie kama kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na kwamba maswali yote yamo.***

Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	**80**	

© 2011, Kamati ya MOKASA

1. UFAHAMU (alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Mkabala wa kuumeni umetawala jamii nyingi za kilimwengu kwa muda mrefu, na jambo hili limesababisha kupuuzwa kwa haki za wanawake kama viumbe kamili. Kauli za kidini na kitamaduni zimetumiwa kushadidia uwezo wa wanaume kuwadunisha wanawake. Hali ya uhusiano kati ya wanawake na wanaume (umenke) imeshughulikiwa katika fasihi kufuatia nadharia ya mtazamo-kike. Hii ni nadharia inayokinzana na mikabala ya kuumeni inayoonekana kupendelea wanaume na kuwanyanyasa wanawake.

Nadharia ya mtazamo – kike ina mielekeo mingi kutegemea itikadi na falsafa ya mhakiki. Kwa mfano, kuna mielekeo mikali hasa inayotoka Marekani, inayochukulia kwamba mwanamume ni adui ya mwanamke na kamwe mwanamume hawezi kushiriki katika ukombozi wa mwanamke. Mielekeo hii inaunga mkono ndoa za jinsia moja. Wafuasi wake wanadai kuwa mwanamke anaweza kushirikiana na wanawake wenzake tu.

Mwelekeo mwingine ni ule unaochukulia kwamba tofauti za kimaumbile baina ya mwanamke na mwanamume si muhimu zilinganishwapo na mshabaha wao. Wanaume wenye itikadi ya kimaendeleo wanaweza kuchangia katika ukombozi wa wanawake, na wanawake wenye itikadi za kijadi wanaweza kushiriki katika kuwakandamiza wanawake wenzao. Kuna mielekeo mingine inayosisitiza nafasi ya uchumi na uundaji wa matabaka baina ya wanawake na wanaume. Yaani mielekeo hii inafungamanishwa na ukombozi wa kiuchumi na ukombozi wa mwanamke.

Kuna wanafasihi kadhaa ambao wanatambua nafasi ya mwanamke katika jamii. Madai makuu ya waandishi hawa ni kwamba mwanamke anakandamizwa pamoja na wafanyakazi wa kiume kwa kulipwa mshahara duni. Pia, akiwa miongoni mwa wafanyakazi wenzake wanaume, ananyanyaswa kwa sababu ya maumbile yake.

Maswali

(a) Ipe taarifa hii anwani mwafaka. (al. 1)

(b) Fafanua jinsi mwanamke alivyodhulumiwa kazini. (al. 2)

(c) Kwa nini mwelekeo wa wamerikani kuhusu mwanamme unachukuliwa kuwa Mwelekeo mkali? (al. 3)

(d) Linganisha wanawake wenye itikadi za kijadi na wanaume wasio na itikadi za kimaendeleo. (al. 2)

(e) Eleza mielekeo ya nadharia ya mtazamo kike. (al. 3)

(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika ufahamu. (al. 4)
   (i) Nadhari
   (ii) Mkabala
   (iii) Itikadi
   (iv) Mhakiki

2. MUKHTASARI (ALAMA 15)

Soma makala haya kisha ujibu maswali.

Lugha ya Kiswahili imepitia hatua nyingi hadi sasa. Baada ya Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia, Waafrika waling'amua kuwa nguvu za pamoja zilihitajika kwa mataifa yote ya Kiafrika ili kuweza kuwang'oa mabeberu mamlakani. Kwa sababu hiyo, Kiswahili kiliteuliwa na kutambuliwa kama lugha ya kuwaunganisha Waafrika katika Afrika ya Mashariki.

Kufikia mwaka wa 1925, wataalamu wa elimu katika Afrika ya Mashariki walitambua Kiswahili kama lugha ya elimu katika eneo hilo. Katika kipindi hiki Kiswahili kilikuwa kikitumiwa kwa mapana na marefu na Waswahili, wafanya biashara wa kiarabu na wamishonari. Kufikia mwaka wa 1930, wakoloni waliunda kamati ya lugha ya Kiswahili ili kusanifisha lugha ya Kiswahili kwa kutumia lahaja ya kiunguja. Kamati hii ilifanya juhudi ya kusawazisha matamshi na matumizi ya lugha ya Kiswahili.

Baada ya Kenya, Uganda na Tanzania kupata uhuru, Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) iliyokuwa na makao yake katika Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam ilianzishwa mnamo mwaka wa 1964. Taasisi hii pamoja na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) liliendeleza harakati za usanifishaji wa Kiswahili. Nchi ya Tanzania iliendelea kuinua hadhi ya Kiswahili kwa kukitumia katika shughuli zote za serikali na kukomesha matumizi ya kiingereza. Kenya kwa upande wake ilikifanya Kiswahili kuwa lugha ya taifa na kiingereza lugha rasmi.

Hata hivyo, wataalam wengi wanahimiza kuwa sharti nchi ya Kenya iwe na sera maalum ya lugha ya Kiswahili. Kwa sababu hiyo, Kiswahili kimefanywa kuwa lugha ya taifa na vilevile lugha rasmi. Isitoshe, vyombo vya habari kama vile runinga, redio na magazeti hutumia Kiswahili kwa kiwango kikubwa.

Ingawaje nchi ya Kenya imejaribu kukikuza Kiswahili, kuna haja ya kuwa na mikakati kabambe ya kukiimarisha Kiswahili. Serikali inaweza kutenga kasima fulani ambayo inaweza kutumiwa kusaidia ukuzaji wa Kiswahili katika taasisi za elimu. Wachapishaji nao wanapaswa kuhimizwa kuchapisha machapisho ya lugha ya Kiswahili. Serikali inaweza kuzuka na vivutio vya kuwafanya wachapishaji hao wasichelewe kuchapisha vitabu hivyo. Waandishi bora wanaweza kutuzwa ili kusaidia ukuzaji wa Kiswahili. Kuna haja pia ya kuwepo kwa vipindi vingi zaidi vya Kiswahili katika redio na runinga.

Zaidi ya hayo, kuna umuhimu wakuwahimiza raia kutambua kuwa Kiswahili ni msingi muhimu wa kujitambulisha kama raia wa nchi hii. Walimu nao wanapaswa kutilia mkazo ufundishaji ufaao wa Kiswahili na waandae makongamano mengi ya fasihi na lugha ili kuwafaidi wanafunzi. Walimu waliohitimu na wanaofunza darasani washirikishwe katika utunzi wa maswali ya mitihani ya kitaifa. Hii ni kwa sababu baadhi ya maswahili yaliyotungwa katika mitihani ya kitaifa huwavunja wanafunzi moyo na kuwafanya wachukie Kiswahili kwa hali na mali.
Tukienzi, tukikuze, tukitambue na tujivunie lugha ya Kiswahili.
Maswali

(a) Fupisha aya tatu za kwanza. (maneno 60 – 65) (al. 5 Mtiririko al. 2)
(b) Eleza mikakati inayostahili kuchukuliwa na nchi ya Kenya ili kuimarisha lugha ya Kiswahili (maneno 65 – 75) (al. 7, utiririko al. 1)

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

(a) Eleza tofauti kati ya sauti hizi. (al. 1)
/w/ na /r/
(b) Tunga sentensi moja iliyo na silabi mwambatano na uipigie mstari. (al. 1)
(c) Bainisha aina za vitenzi katika sentensi zifuatazo : (al. 2)
(i) Shangazi alikuwa angali analima shambani.
(ii) Yeye ndiye mwanafunzi aliyepokea tuzo.
(d) Tunga sentensi moja kubainisha maana mbili tofauti za neno : (al. 2)
Randa

(e) Taja vipashio vya lugha ya Kiswahili. (al. 2)

(f) Bainisha viambishi tamati na ueleze dhima yake katika neno lifuatalo. (al. 2)
Wasomapo

(g) Tunga sentensi moja ukitumia nomino ya dhahania na nomino ya wingi. (al. 2)

(h) Tumia neno 'Yule' kama kivumishi na kirejeshi katika sentensi moja. (al. 2)

(i) Ainisha mofimu katika sentensi;
Ajuza afa. (al. 2)

(j) Tunga sentensi moja ili kudhihirisha matumizi ya kiambishi '-ndi-' na ueleze matumizi yake. (al. 2)

(k) Andika katika usemi halisi. (al. 2)
Mama alimshurutisha Maria kuandika meza.

(l) Andika upya sentensi ifuatayo kwa kuzingatia kauli iliyowekwa mabanoni. (al. 2)
Wanafunzi wale ni watundu na kwa hivyo ; itakuwa vigumu kusomesha darasa hilo (kutendesheka)

(m) Ainisha shamirisho katika sentensi hii. (al. 2)
Mama alinipikia pilau.

(n) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali. (al. 4)
Lile liumala ndilo ling'olewalo.

(o) Badilisha sentensi ifuatayo katika hali ya udogo na ukubwa. (al. 2)
Mwanamke mnene alipatikana akimshonea nguo mwanamume mweusi.

(p) Tunga sentensi itakayodhihirisha matumizi ya kihisishi cha makubaliano. (al. 1)

(r) Weka kibainishi panapostahili katika sentensi ifuatayo. (al. 1)
Mimi na Pendo tutaenda shuleni.

(s) Eleza maana tofauti kati ya sentensi zifuatazo. (al. 2)
(i) Mama angefika angelinunulia nguo.
(ii) Mama angalifika angalininunulia nguo.

(t) Tunga sentensi kuonyesha hali ya mazoe ya kutendeka kwa jambo katika hali timilifu. (al. 2)

(u) Ainisha viwakilishi nafsi katika sentensi hii. (al. 2)
Mimi ndimi Bwana Mungu wako, usiabudu miungu mingine.

(v) Tambua kirai nomino na kishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo. (al. 2)
Mwalimu mwenyeji amehamia shule iliyoanzishwa mwaka uliopita.

4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)

(a) Eleza maana ya dhana zifuatazo. (al. 5)
Sajili
Kaida
Lugha
Ujozi-lugha
Lingua franka

(b) Huku ukitoa mifano eleza sifa zozote tano zinazotambulisha rejista ya michezo. (al. 5)